

**Sehemu ya 2 – Semina ya 2  
Damu na Moto!**

**Kwa kuwa sasa umeanza vizuri, unahitaji nguvu ya kumaliza mashindano.**

**Sura ya 8-11 zinazungumzia:**

8.     **Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano - Utangulizi**
9.     **Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano - Msalaba**
10.    **Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano - Ukombozi**
11.    **Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano - Ubatizo katika Roho Mtakatifu**

## Sura ya 8 - Nguvu ya Kupiga mbio katika Mashindano – Utangulizi

Katika Sehemu ya kwanza ya kitabu hiki, sura 7 za kwanza, tulijifunza kwamba lipo tumaini kwetu sisi tusioweza kupata tumaini katika “mfumo wa dunia”. Tuliona kwamba tukiacha kuutegemea ulimwengu, ufalme wa Mungu utakaribia (utakuwa karibu nasi).

Tulijifunza kwamba Yesu alifundisha katika Marko 4:11 kwamba siri ya ufalme wa Mungu imo ndani ya mfano wa mpanzi. Alifundisha kwamba Neno la Mungu ni mbegu, mioyo yetu ni udongo na matokeo yake ni matunda.

Matunda yatabadilisha tabia zetu zifanane na tabia ya Yesu, yatatupa mahitaji yetu binafsi na pia yatusukuma kwenda katika ulimwengu unaoangamia kuzaa matunda ya uzima wa milele kwa ajili ya wengine.

**Tulijifunza kwamba mbegu hupitia hatua nyingi ili kuwa tunda halisi  
Hii hapa ndiyo dhamira ya kitabu cha “Kukua au Kufa.”**

- 1) Tunahitaji kuugeukia ufalme wa Mungu na Neno ili tuzae matunda.
- 2) Tunahitaji kujua jinsi ya kuwa na urafiki wa karibu na Mungu - yaani Mto Utirikao.
- 3) Tunahitaji kujua jinsi ya kutoka na kukaa mbali na hali ya kuwa Wafungwa katika nchi ya Ahadi.
- 4) Tunahitaji kujua zaidi tabia ya Mungu - Mungu ni Nani
- 5) Tunahitaji kujua sisi ni akina nani katika Kristo - KUKAA.
- 6) Tunahitaji kuubeba msalaba wetu na kuenenda katika hali ya kultii Neno - KUENENDA.
- 7) Tulijifunza katika somo la KUPINGA kwamba kuna adui wa kiroho anayepinga mambo yote hayo. Huyu ni Shetani na pepo wake. Tulijifunza kwamba tunahitaji uvumilivu na nguvu ya kumpinga adui huyu hadi matunda yanapopatikana. Kwa maneno mengine, tunahitaji kumngojea Bwana aje aitimize ahadi. “Ili msiwe wavivu, bali mkawe wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa imani na uvumilivu” (Waebrania 6:12).

Namshukuru Mungu iwapo umeyashika mambo hayo yaliyoletwa kwetu kwa njia ya Neno la Mungu. Kama umefanya hivyo, unahitaji nguvu katika maisha yako ili kukamilisha hatua na kuona udhihirisho wa matunda katika maisha yako.

Kama jinsi mimea inavyohitaji maji na mbolea ili ipate nguvu hadi inapozaa matunda, sisi pia tunahitaji nguvu. Sehemu ya 2 imelenga kukusadia kufahamu jinsi ya kujitwalia nguvu hii.

## Maisha yetu katika Kristo sio uzoefu, bali ni mashindano.



**Ni jambo zuri kuanza mashindano**, hata hivyo tunahitaji kujua jinsi ya kumaliza. Watu wengi huanza lakini hawamalizi. Tunahitaji **nguvu** ya kumaliza mashindano vinginevyo tutashindwa. Katika Waebrania 12:1 tunaambiwa hivi: “Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila **mzigo** mzito, na **dhambi** ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale **mashindano** yaliyowekwa mbele yetu.”

### **Maandiko yanatuambia kuwa nguvu tunayohitaji inapatikana katika:**

**1. Msalaba au damu ya Yesu.** “Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuzi, bali kwetu sisi tunaoolewa ni nguvu ya Mungu” (1 Wakorintho 1:18).

**2. Nguvu ya Mungu ya kukomboa.** “Alipokuwa katika kumwendea, pepo akambwaga chini, akamtia kifafa. Yesu akamkemea pepo mchafu, akamponya mtoto, akamrudishia babaye. Wote wakashangaa, wakuiona ukuu wa Mungu” (Luka 9:42,43a).

**3. Ujazo wa Roho Mtakatifu.** “Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi” (Matendo 1:8).

**Mungu hakutuacha yatima hapa duniani** tujihudumie wenywewe hadi tutakapokufa na kwenda mbinguni. Mungu ni mwenye busara. Ana njia ya kututunza, lakini wengi hawaijui njia hiyo. “Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu” (Yohana 14:18). Yesu alikuwa akizungumzia kuja kwa Roho Mtakatifu. Katika sura zifuatazo tutaangalia jinsi Roho Mtakatifu alivyo muhimu katika kutufanya tusiwe yatima au watu wasio na msaada katika dunia hii.

**Msalaba wa Yesu ndio uliomshinda Shetani** na kutupatia ushindi. Hiyo ni nguvu. Tukiutendea kazi ukweli wa Msalaba tunapata nguvu. Hata hivyo, nakubali kwamba ukweli wa msalaba hauwezi kuonekana kikamilifu katika maisha yetu pasipo nguvu inayozungumzwa katika Mdo 1:8, yaani ujazo wa Roho Mtakatifu.

**Kwa mfano**, nguvu ya kuwashaa taa katika jengo hutokana na jenereta inayotengeneza umeme. Unaweza kusimama kando ya soketi ukutani na kuifurahia soketi hiyo huku ukijua kwamba ina nguvu ndani yake. Hata hivyo usipochomeka kifaa cha umeme kwenye soketi hiyo, utakuwa bado hujafaidika

na nguvu ya umeme. **Tutachunguza kuhusu ukweli** wa nguvu ya msalaba, na pia tutachunguza jinsi ya kuufanya ukweli huo uwe wako binafsi katika maisha yako.